

Usaidizi wa **Section 4 NASS***

Je! Usaidizi wa **Section 4*** ni wa nani?

Unaweza kustahiki usaidizi wa **Section 4*** ikiwa yote yafuatayo yanatumika:

- Ulikuwa mtafuta uhamisho na
- Umenyimwa madai yako ya uhamisho na
- Hauna njia zingine za usaidizi
- Ikiwa umekata rufaa unastahili usaidizi. Tafadhali tuulize.

Na ikiwa mojawapo ya yafuatayo inatumika:

- Tayari umeomba hati za kusafiri (kutoka kwa ubalozhi wako/Huduma ya Uhamiaji) au umejiandikisha Kurudi kwa lhari na unasubiri maelezo ya kusafiri yakamilishwe kabla ya kurudi
- Hauwezi kimwili kusafiri nje ya Uingereza kwa sababu za kimatibabu
- **Home Office*** inasema hakuna njia salama ya kurudi nchini mwako
- Umepewa rufaa ya kufanya **Judicial Review*** inayohusiana na madai yako ya uhamisho
- Ofisi ya Nyumbani husema haki zako za kibinadamu zitakiukwa ukiwa hauna usaidizi - kwa mfano, kwa sababu wakili wako amefanya **further representations*** kwa madai yako ya uhamisho au kwa sababu uko kizuizini

Je! Usaidizi wa **Section 4*** ni nini?

- Nyumba hutolewa na **NASS*** pamoja na vocha ya £35 kwa kawaida kila wiki kwa ajili ya chakula na vifaa vya kujipambua
- Hakuna usaidizi zaidi wa kifedha
- Nyumba inawezakuwa katika eneo lako lakini inaweza kukubidi uhame kutoka kwa nyumba yako ya sasa
- **NASS*** inaweza kuangalia mara kwa mara ili ione ikiwa bado unafikia vigezo vilivyo hapo juu, na inaweza kukomesha usaidizi ikiwa haufikii (k.v. ukiondoa maombi yako ya Kurudi kwa lhari, usaidizi wako unaweza kughairiwa).

Ninapaswa kuomba aje?

- Tafadhali enda kwa chombo chako cha ushauri kilicho karibu - kinaweza kukusaidia kujaza fomu ya kuomba kwa **NASS***
- **NASS*** itakuuliza kutia saina fomu inayosema kwamba unaelewa masharti ya usaidizi wa **Section 4*** - tutakufafanulia haya.
- Baada ya kuomba, inaweza kuchukua muda kabla ya kujua ikiwa **NASS*** itakupatia usaidizi wa **Section 4***.
- Ikiwa **NASS*** itakupatia usaidizi wa **Section 4***, inaweza kuchukua wiki ingine kabla ya wewe kuweza kuhamia nyumba hiyo.

*Maneno haya ni majina ya Kiingereza ya mashirika au maneno mengine ambayo hayawezi kutafsiriwa. Tafadhali muulize mfanyakazi wa ushauri akufafanulie maana yake.

Tafadhali tuulize ikiwa una maswali yoyote au jambo lolote.